



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE WA**  
**JIMBO LA MBARALI NA MADIWANI KATIKA**  
**KATA SITA ZA TANZANIA BARA**

Dodoma, 5 Agosti, 2023

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiitaarifu Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Mbarali, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali Mkoa wa Mbeya. Nafasi hiyo wazi inatokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mhe. Francis Leonard Mtega. Spika ametoa taarifa hiyo kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Aidha, Tume imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa, akiitaarifu juu ya uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika kata sita za Tanzania Bara. Waziri ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Kutokana na taarifa hizo, Tume kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 inatoa taarifa kwa umma kuhusu uwepo wa uchaguzi mdogo wa Ubunge wa Jimbo la Mbarali na Madiwani katika kata sita za Tanzania Bara.


Kata zinazohusika na uchaguzi huo mdogo ni kutoka halmashauri sita zilizopo katika mikoa minne kama ifuatavyo: -

Na.	Mkoa	Na.	Halmashauri	Kata
1.	Dodoma	1.	Jiji la Dodoma	Nala
2.	Ruvuma	2.	Manispaa ya Songea	Mfaranyaki
		3.	Wilaya ya Madaba	Mtyangimbole
3.	Mwanza	4.	Wilaya ya Misungwi	Mwaniko
4.	Kilimanjaro	5.	Wilaya ya Moshi	Old Moshi Magharibi
		6.	Wilaya ya Rombo	Marangu Kitowo

Ratiba ya uchaguzi mdogo utakaofanyika ni kama ifuatavyo.

Na.	Tukio	Tarehe
1.	Zoezi la utoaji fomu za uteuzi	13/8/2023 hadi 19/8/2023
2.	Uteuzi wa wagombea katika uchaguzi	19/8/2023
3.	Kampeni za uchaguzi	20/8/2023 hadi 18/9/2023
4.	Siku ya uchaguzi	19/9/2023

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi cha uchaguzi huu mdogo.

  
 Kailima, R. K.  
MKURUGENZI WA UCHAGUZI